

Jina la Mwanafunzi _____

Jina la Shule _____

**KEYS EDUCATIONAL AND STATIONERY SERVICES (KESS)
NAMBA YA USAJILI: 473801**



Barua pepe: keyseducationalservices@gmail.com

Simu: 0758587618/0679587618

KIFURU-KINYEREZI, DAR ES SALAAM

**MTIHANI WA KWANZA WA UTAMILIFU DARASA LA NNE
SOMO: KISWAHILI**

Muda: Saa 1:30

Ijumaa 13 Mei, 2022

Maelekezo

1. Mtihani huu una sehemu **A, B, C, D** na **E** zenye jumla ya maswali **matano (5)**
2. Jibu maswali **yote** katika kila sehemu
3. Majibu yote yaandikwe katika karatasi hii
4. Tumia kalamu ya wino wa rangi ya **buluu** au **mweusi**
5. Simu za mikononi na vifaa vingine visivyohitajika **haviruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
6. Andika kwa usahihi **Jina lako** na **Jina la Shule** sehemu ya juu kulia kwenye kona ya kila ukurasa

KWA MATUMIZI YA MTAHINI TU

NAMBA YA SWALI	ALAMA	JINA LA MTAHINI
1.		
2.		
3.		
4.		
5.		
JUMLA		
SAINI YA MWINGIZA ALAMA		
SAINI YA MHAKIKI		



Jina la Mwanafunzi _____
Jina la Shule _____
SEHEMU A (Alama 10)
IMLA

1. Sikiliza sentensi zinazosomwa na msimamizi wa mtihani kisha uziandike kwa usahihi

- i. _____
- ii. _____
- iii. _____
- iv. _____
- v. _____

SEHEMU B (Alama 10)
MISAMIATI

2. Andika maneno yenye maana sawa na maneno haya kwa kuandika jibu sahihi katika sehemu zilizoachwa wazi

Mfano: Dagua – Kauzu

- i. Tembo - _____
- ii. Gari - _____
- iii. Mwisho - _____
- iv. Beseni - _____
- v. Peremende - _____



Jina la Mwanafunzi _____

Jina la Shule _____

SEHEMU C (Alama 10)

METHALI, NAHAU NA VITENDAWILI

3. Jibu maswali yafuatayo kutokana na maelekezo ya kila kipengele kwa kuandika jibu sahihi katika sehemu iliyoachwa wazi

i. Ingawa Chaupole ni mlemavu, hufanya kazi kwa bidii kama watu wengine na hapendi ulemavu umfanye mvivu. Je, ni methali gani inaendana na maelezo haya?

ii. Je, utatumia methali gani kumshauri mtu asiyetaka kushughulikia jambo dogo ambalo mwishowe humletea matatizo makubwa?

iii. Andika nahau ambayo ina maana sawa na neno lililopigiwa mstari katika sentensi hii: Baada ya kusubiri kwa muda mrefu hatimaye **aliamua** kuondoka.

iv. Juma ana mkono mrefu. Nahau “kuwa na mkono mrefu” ina maana gani?

v. Tegua kitendawili hiki: Kamba yangu ndefu lakini haiwezi kufunga mzigo wa kuni

SEHEMU D: (Alama 10)

UTUNGAJI

4. Panga sentensi zifuatazo katika mtiririko mzuri kwa kuzipa herufi A, B, C, D na E. Kipengele cha (vi) kimefanyika kama mfano

i. Hutandika vitanda vyao, huoga na kuvaa sare za shule. []

ii. Hassani, Rozi na Yusufu wanasoma darasa la nne. []

iii. Hunywa chai na kwenda shuleni. []

iv. Hufagia darasa lao na uwanja wa shule. []

v. Huamka mapema kila siku asubuhi. []

vi. Husimama mstarini na kuingia darasani. [**F**]



Jina la Mwanafunzi _____

Jina la Shule _____

(Alama 10)

SEHEMU E: UFAHAMU

5. Soma hadithi ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata kwa kuandika majibu sahihi katika nafasi zilizoachwa wazi

Katika kijiji cha Tupendane aliishi mzee mmoja aliyefahamika kwa jina la Mzee Tola. Mzee Tola alikuwa mchoyo sana. Mara nyingi alipenda kula chakula peke yake huku watoto wake pamoja na mke wake wakishinda na kulala njaa.

Siku moja umeme ulikatika nyumbani kwa Mzee Tola. Kukawa na giza totoro. Hivyo mke wa Mzee Tola aliwaambia watoto wake wasile chakula hadi umeme urudi maana si vyema kula gizani na harakaharaka haina baraka. Mzee Tola aliamua atumie fursa hiyo kuiba chakula na kukila peke yake. Alinyata kuelekea mezani akachukua bakuli iliyojaa minofu ya nyama na kuketi chini ya meza huku akiendelea kufakamia chakula. Baadaye akaona kama anatafuna kitu kigumu na baada ya muda umeme ukarudi. Mzee Tola alijikuta akitafuna konokono. Watoto wake na mke wake Bi Sikitu walimcheka na kumshangaa sana huku wakisema mchoyo hana rafiki na siku za mwizi ni arobaini. Mzee Tola aliona fedheha na kuishia kutapika.

Maswali

i. Mzee Tola alikuwa na tabia gani?

ii. Nahau ipi inaweza kutumika kuelezea tabia ya Mzee Tola?

iii. Mke wa Mzee Tola aliiitwa nani?

iv. Kitu kigumu ambacho mzee Tola alitafuna akiwa gizani kilikuwa ni nini?

v. Hadithi hii inatoa funzo gani?
